

Mikakati yaanika kudhibiti homa ya nguruwe

SERIKALI imekiri kujitokeza mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe katika mikoa kadhaa nchini, na kusababisha hasara kwa wafugaji huku ikianisha mikakati nane itakayofanyika kudhibiti hali hiyo.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akijibu swalii la Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe(CCM) aliyeoji, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa mlipuko wa magonjwa ya Nguruwe hayajitokezi

Akijibu swalii hilo, Naibu Waziri huyo alisema ugonjwa huu unaosababishwa na virusi, hauna chanjo wala tiba. Njia pekee za kudhibiti ugonjwa wa homa ya nguruwe ni kuzingatia kanuni bora za ufugaji wa nguruwe.

Alibainisha kuwa Serikali na wadau wengine inafanya jitihada za kudhibiti ugonjwa huu ambazo ni pamoja na kuhimiza wafugaji kuacha kufuga nguruwe kwa njia huna (scavenging), kuzuia wageni kuingia kwenye mabanda ya nguruwe.

Auth: Kuhimiza wafugaji wanulizie

dawa za kuua virusi na kupe kwenye mabanda na kuweka dawayakuchovya kwenye milango ya mabanda, Kuweka katazo la kusafirisha nguruwe na mazao yake kutoka sehemu zenyewe ugonjwa.

Pia, Kuhimiza wafugaji kutokuruhusu wachinjaji au wafanyabiashara kuingia katika mabanda na kuchagua nguruwe wa kununua. Wafugaji kuepuke kulisha nguruwe mabaki ya vyakula kutoka kwenye hotelini na migahawa.

Nyingine, ni kuacha kuchanganya

banda moja na wafugaji kutoa taarifa za ugonjwa au vifo vya nguruwe pindi inapojitokeza kwa Mtaalamu wa Mifugo aliye karibu.

"Mkakati wa Serikali kupitia Wizara ni kuendelea kutoa elimu ya udhibiti kwa wadau wote katika mnyororo wa thamani, wakiwemo wafanyabiashara na wasafirishaji wa nguruwe pamoja na watoa huduma za Afya ya Mifugo.

"Kazi hii tunaendelea kuifanya kwa kuzingatia uhalisia katika kila eneo kwa wafugaji wakubwa na wadogo," alisitiza Naibu Waziri huyo.

HABARI

JKT yatekeleza agizo la Rais Samia kuzalisha vifaranga vya Samaki

**NA IMMACULATE RUZIKA,
MOROGORO**

KAMATI ya kimkakati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) limeanza kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuzalisha vifaranga vya Samaki kwa ajili kuboresha ufugaji wa samaki wenye tija.

Aidha utekelezaji huo unafanyika katika Kikosi Cha Jeshi la Kujenga Taifa 837 JKT Chita ambao wameanza kutekeleza agizo la Rais Samia la kutaka uzalishaji wa vifaranga vya Samak uwe kwa wingi ili kukuza Sekta ya ufugaji wa Samaki.

Katika Hotuba yake aliyoitoa mapema mwezi huu Ikulu Chamwino jijini Dodoma Rais Samia alitoa agizo la uzalishaji wa vifaranga vya Samaki kwa wingi uli kuboresha ufugaji wa samaki wenye tija.

Akizungumza jana ka-

tika Kambi ya 837 JKT Chita iliyopo Mlimba mkoani hapa mtaalamu wa Samaki Luteni Joseph Lyakurwa alisema wameanza utekelezaji wa agizo la Rais kwa kujenga mabwawa 26 ya kufugia samaki.

"Tumeanza kutekeleza agizo la Rais Samia kwa kujenga matenki ya Saruji 26 ya kufugia samaki ambayo tunataraja kuzalisha vifaranga zaidi ya 200,000 kwa mwezi," alisema Luteni Lyakurwa.

Aidha Luteni Lyakurwa alisema JKT imetenga hekali 14 kwa ajili ya ya mradi huo ambao pia maji yatakayotoka katika matenki hayo yatakuwa ya umwagiliaji katika mashamba ya mpunga.

"Hapa hakuna kitaka-choachwa haya Maji unayoona hapa kwenye Tanki yanaingia na kutoka hivyo, yanapotoka katika matenki yanakuwa na mbolea hivyo tunatumia kumwaqilia

mashamba," alisema Luteni Lyakurwa.

Vilevile Luteni Lyakurwa alisema mbali na ufgaji huo lakini wanatoa elimu kwa vijana wa JKT wanaojitolea pamoja na wanafunzi kutoka Vyuo vya Elimu ya juu ambao wanaenda kufanya mafunzo ya vitendo.

Aidha Luteni huyo

alisema maeneo hayo ni rafiki kwa mazingira kwani wanatunza rasili-mali Ardhi na Maji yanayotoka katika maporomoko ya Milima ya Kilombero.

Hata hivyo mtalaamu huyo alisema kwa kuanzia wametumia hekali mbili ambazo wana-tumia kuzalisha vifaranga

bora ambao watatatua Changamoto ya upungufu wa vifaranga vya Samaki.

Naye mmoja wa vijana wa kujitolea waliopo katika Kikosi hicho Barakati Mlugu alisema amefaidika kutokana na mafunzo hayo ya Jeshi ikiwemo ufgaji, na Ujenzi wa Mabwawa ya samaki.

*Kaimu Kamanda
wa Kikosi Chita
JKT 837 Meja
Evergreen Bartaz-
ary alipokuwa
akitoa maelezo
kuhusu miradi
inayoendeshwa
Kikosini hapo*



Mikakati kudhibiti homa ya nguruwe yawekwa bayana

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeainisha mikakati minane iliyofanyika kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe uliojitokeza hivi karibuni katika mikoa kadhaa na kusababisha hasara kwa wafugaji.

Naibu Waziri Abdallah Ulega, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swal la Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe.

Mwambe alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha kuwa mlipuko wa magonjwa ya Nguruwe haujitokezi mara kwa mara nchini.

Ulega akijibu swal hilo, alisema ugonjwa huo unaosababishwa na virusi, hauna chanjo wala tiba na kwamba njia pekee za kudhibiti ni kuzingatia kanuni bora za ufugaji wa nguruwe.

Alibainisha kuwa serikali na wadau wenigne inafanya jitihada za kudhibiti ugonjwa huo ambazo ni pamoja na kuhimiza wafugaji kuacha kufuga nguruwe kwa njia huria, kuzuia wageni kuingia kwenye mabanda ya nguruwe.

Pia mkakati mwininge ni kuhimiza wafugaji wapulizie dawa za kuua virusi na kupe

kwenye mabanda na kuweka dawa ya kuchovya kwenye milango ya mabanda, kuweka katazo la kusafirisha nguruwe na mazao yake kutoka sehemu zenyе ugonjwa.

"Kuhimiza wafugaji kutokuruhusu wachinjaji au wafanyabiashara kuingia katika mabanda na kuchagua nguruwe wa kunnua, wafugaji kuepuke kulisha nguruwe mabaki ya vyakula kutoka kwenye hotelini na migahawa," alisema.

Nyingine ni kuacha kuchanganya nguruwe wageni na wenyiji kwenye banda moja na wafugaji kutoa taarifa za ugonjwa au vifo vya nguruwe pindi inapojitokeza kwa Mtaalamu wa Mifugo aliye karibu.

Hata hivyo, alisema mkakati wa serikali kupitia Wizara ni kuendelea kutoa elimu ya udhibiti kwa wadau wote katika mnyororo wa thamani, wakiwamo wafanyabiashara na wasafirishaji wa nguruwe pamoja na watoa huduma za afya ya mifugo.

"Kazi hii tunaendelea kuifanya kwa kuzingatia uhalsia katika kila eneo kwa wafugaji wakubwa na wadogo," alisisitiza.

NIPASTIE 7 UK 7, APRIL 24, 2021

Ndaki directs NARCO to set aside 15,000 acres for Mpeta, Chakulu villagers

By Guardian Correspondent, Kigoma

LIVESTOCK and Fisheries Minister Mashimba Ndaki has directed the National Ranching Company (NARCO) to set aside 15,000 acres of the ranch area to be allocated to people of two villages - Mpeta and Chakulu in Uvinza District, Kigoma Region in order to resolve a long time land conflict pitting the ranch and villagers.

Ndaki issued the directives on Sunday during his visit in Uvinza District aimed to resolve the land conflict following unlawful invasion of the ranch area by the residents of the two villages.

Speaking at different times to the residents of the two villages, Ndaki said the government has decided to reach the decision to enable the villagers concentrate themselves on development activities and put behind them the land conflict.

He added: "After the land reallocation exercise is complete, the Uvinza District Commissioner and his team will go to the areas for evaluation for the purpose of formalisation of the allocated land

plots."

He stressed that even though the villagers had contravened the laws, the government has looked into wide interests of the villagers, hence it decided to set aside part of the ranch area to enable them live in peace and engage themselves in economic activities for their wellbeing.

"This ranch is for livestock keeping and is not for human settlements, whoever will try to invade it for the purpose of dwelling or cultivation will be committing a crime and will be prosecuted, and if anyone want to graze his livestock, come to us, we shall rent him an area for the purpose," said the minister.

After thanking the minister for the decision, Uvinza District Commissioner Mwamanvua Mrindoko stressed to the villagers to avoid conflicts that were not beneficial to them.

For his part, the Chakulu Village Chairman, Mohamed Baswage thanked the government for giving areas of land to the villagers, saying the decision will assist them to pursue economic activities for their own wellbeing.

“

This ranch is for livestock keeping and is not for human settlements, whoever will try to invade it for the purpose of dwelling or cultivation will be committing a crime and will be prosecuted, and if anyone want to graze his livestock, come to us, we shall rent him an area for the purpose